

TAARIFA KWA WADAU KUHUSU UMUHIMU WA MIHTASARI YA MASOMO

Wadau wengi wamekuwa wakiulizia umuhimu na upatikanaji wa mihtasari ya masomo yafundishwayo katika shule na vyuo vya ualimu nchini. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania inaandaa mitaala ya elimu kwa masomo ya Elimu ay Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

1.0 Maana ya Muhtasari wa Somo

Muhtasari wa somo ni kitabu au mwongozo unaoonyesha maarifa, stadi na ujuzi wa somo ambao mwanafunzi anatakiwa kujifunza katika ngazi mojawapo ya elimu. Ni kitabu pekee cha kitaaluma na kitaalamu kinachotumiwa na mwalimu, mwanafunzi na wanataaluma wengine ili kutambua mambo ambayo yanapaswa kufundishwa kwa kufuata mtiririko uliooneshwa. Muhtasari wa kila somo linalofundishwa shuleni unatayarishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania na kuidhinishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

2.0 Yaliyomo Katika Muhtasari

Muhtasari una maelezo ya kina kama vile utangulizi, malengo na ujuzi unaopaswa kufikiwa kwa kila darasa.

Kila muhtasari una sehemu ya utangulizi ambapo yafuatayo yameelezwa kwa muhtasari:

Malengo ya elimu Tanzania, malengo ya ngazi ya elimu husika, malengo ya kufundisha somo, ujuzi wa somo, mada za muhtasari, mbinu za kufundishia/kujifunzia somo, zana/vifaa vya kufundishia, upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi na idadi ya vipindi. Pia kwa kila darasa vimeonyeshwa vipengele kama mada ndogo, malengo mahsusuni, mbinu za kufundishia/kujifunzia, vifaa/zana, upimaji na vipindi.

3.0 Umuhimu wa Mihtasari ya Masomo

- (a). Muhtasari wa somo ni mwongozo pekee wa kitaaluma na kitaalamu katika somo kwa ajili ya wadau wa elimu hususan mwalimu na mwanafunzi kuelewa kinachopaswa kufundishwa au kujifunza.
- (b). Matayarisho ya walimu kufundisha wanafunzi darasani hufanyika kwa kuchukua vipengele vya muhtasari na kuvitumia. Mfano andalio la somo na azimio la kazi huandikwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo.
- (c) Kila mwalimu na pia wanafunzi wakiwemo wadau wengine wanapaswa kufahamu yaliyomo katika mihtasari ili kuweza kufikia malengo ya elimu yaliyopangwa. Hivyo kila mwalimu anapaswa kuwa na muhtasari wa somo lake na kuutumia wakati wote.
- (d) Muhtasari wa somo ni kisima cha yote yanayotarajiwa kumfikia mtoto. Pia mihtasari ni daraja kati ya mwalimu, vitabu, vifaa vya kufundishia na mwanafunzi.

(e) Mitihani ya wanafunzi katika ngazi ya shule wilaya na kitaifa, hutungwa kupima maarifa yaliyoandikwa katika mihtasari.

4.0 Upatikanaji wa Mihtasari ya Masomo

Mihtasari ya masomo yanayofundishwa katika shule za Awali na Msingi, Sekondari (O-level na A-level) na vyuo vya ualimu (Cheti na Stashahda) inapatikana Taasisi ya Elimu Tanzania ikiwemo iliyotafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza kwa ajili ya shule za Awali na Msingi. Kwa mahitaji ya shule, walimu, wanafunzi, asasi mbalimbali na maduka ya vitabu, tafadhali wasiliana au agiza kwa kutumia anwani zifuatazo: Mkurugenzi, Taasisi ya Elimu Tanzania, S.L.P 35094 Dar es Salaam: Simu Na: 022 2773005; Faksi Na: 022 2774420; E-mail: director.tie@tie.go.tz au tembelea tovuti www.tie.go.tz

5.0 Ushauri kwa wadau wote

Wadau wengi wakiwemo wazazi hawajui umuhimu wa mihtasari. Aidha wadau wengi hawajui elimu inayotolewa kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali ili kuweza kutoa ushauri kwa walengwa na pia kuchangia kikamilifu katika kutoa elimu bora kwa watoto wao.

Aidha uelewa wa mihtasari uasaidai wazazi kufuatilia elimu ya watoto wao darasani na kuziba mapengo pale ambapo uelewa, ufundishaji, ujifunzaji au vifaa havitoshelezi.

Ili kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya elimu Tanzania unashauriwa kujipatia kujipatia nakala ya mihtasari ya masomo mbalimbali kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

6.0 Mawasiliano

Kwa mahitaji yako wasiliana na: Mkurugenzi, Taasisi ya Elimu Tanzania, S.L.P 35094 Dar es Salaam: Simu Na: 022 2773005; Faksi Na: 022 2774420; E-mail: director.tie@tie.go.tz au tembelea tovuti www.tie.go.tz

Dkt. Paul S.D. Mushi
Mkurugenzi
Taasisi ya Elimu Tanzania¹

¹ Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti: www.tie.go.tz na toa maoni kupitia barua pepe: mafunzo@tie.go.tz